



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

## **MRADI WA UPANUZI WA MFUMO WA UZALISHAJI NA UGAWAJI MAJI CHALINZE AWAMU YA TATU**

Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa (Mb) leo atafanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji wa awamu ya tatu ya upanuzi wa chanzo na mtandao wa maji wa Chalinze unaotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia DAWASA.

Katika ziara hiyo Mh. Waziri anatarajiwa kutembelea kazi mbalimbali zinazoendelea ikiwemo shughuli za upanuzi wa chanzo, ujenzi wa matenki, ulazaji mabomba, ujenzi wa vituo vya kuchote maji pamoja na ujenzi wa ofisi mpya ya uendeshaji wa mradi huo.

Mradi utahusisha upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji wa Chalinze ambao chanzo cheke ni mto Wami. Lengo la ni kuongeza uzalishaji kufikia mita za ujazo 900 kwa saa kutoka mita za ujazo 500 kwa saa.

Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa Matenki 19, ulazaji wa mabomba ya ukubwa mbalimbali umbali wa jumla ya kilometa 1,022, ujenzi wa vizimba vya kuchota maji 351 katika vijiji na vitongoji vya Halmashauri za Chalinze na Bagamoyo. Vizimba vingine vitajengwa katika baadhi ya maeneo ya Halmashauri za Handeni – Tanga na Ngerengere – Morogoro.

Mradi huu ni mkubwa na unahusisha baadhi ya maeneo ya Mikoa wa Tanga, Morogoro na Pwani. Kazi hii itakapokamilika, wakazi waliopo maeneo ya Manga hadi Tengwe katika Mkoa wa Tanga; mji na vitongoji

vya Chalinze na baadhi ya maeneo ya Bagamoyo na Kibaha katika Mkoa wa Pwani watafaidika. Mradi pia utanufaisha baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Morogoro ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kizuka A na B, Ngerengere, Kinoko A and B, Tukamisasa, Lulenge, Visakazi hadi Bwawani pamoja na Sangasanga A na B,

Maeneo mengine yatakapojengwa matenki ni Pamoja na Pera, Pingo Bwilingu, Msoga, Diozile, Lugoba, Mindutulieni, Saleni, Mazizi, Msata, Kihangaiko, Kilemera, mandera, Hondogo, Miono, North 3, Kimange, Rupungwi na Manga. Kati ya hayo matenki 19 mojawapo ni tenki kuu la Mazizi lililo na uwezo wa kuhifadhi lita Milioni 2.

Hadi utakapokamilika, mradi utagharimu dola za Marekani 41,362,023.43 ambazo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya EXIM ya India. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwoshoni mwa mwaka 2018.

**Imetolewa na**

**Ofisi ya Uhusiano wa Jamii**

**DAWASA**